**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA MOMBA**

SHULE YA SEKONDARI CHIKANAMLILO,
S.L.P 210,
**TUNDUMA-MOMBA.**

TAREHE…………………..

**SIMU ZA KIGANJANI**
● ***Mkuu wa shule:*** *+255 767 au 735 600 121 (Barua pepe: makungachristian989@gmail.com)*
● ***Makamu Mkuu wa shule:*** *+255 656 320 048*
● ***Matron:*** *+255 763 639 222*
● ***Simu ya mezani:*** *+255 710 533 855*

**KUMB.NA: CHIKANAMLILO S.S/JIFV-2022/VOL1/001**

KWA MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI……………………………………………………………………………………………
S.L.P……………………………………………………………………………………………………………………………..
……………………………………………………………………………

Ndugu;

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA MASOMO YA KIDATO CHA TANO CHIKANAMLILO SEKONDARI TAHASUSI YA "CBG" 2022/2023**

Ninayo heshima na furaha kubwa kukutaarifu kuwa; mwanao amechaguliwa kujiunga na masomo ya Elimu ya Kidato cha Tano kwa tahasusi (Combination) tajwa hapo juu kwa mwaka 2022/2023. Haya ni matokeo chanya ya jitihada zake, walimu wake na nidhamu nzuri ya kijana wako. Aidha; Malezi bora kwa mwanao yamechangia kufikia hatua hii muhimu ya kitaaluma.


Shule itafunguliwa tarehe ……/07/2022. Mwanao anapaswa kufika tarehe tajwa kuanza masomo. Na usajili unaanza tarehe… /07/2022. Hivyo; aripoti kwa wakati uliopangwa.

Shule imesajiliwa kwa namba S.881. Na inapatikana Mkoa wa **SONGWE**, Halmashauri ya Wilaya **MOMBA**, Tarafa ya **NDALAMBO**, Kata ya **NDALAMBO**. Ipo umbali wa kilomita Hamsini (50) kutoka mji wa biashara wa **TUNDUMA** kando ya njia kuu ya **TUNDUMA-SUMBAWANGA**. **Nauli kutoka Tunduma hadi Ndalambo (Ilipo shule) ni Tsh. 2,500/= (Kwa Hiace) ama Tsh. 3,000/= (Kwa Bajaj au mabasi yaendayo Sumbawanga).**

Unashauriwa kukamilisha ada na michango ya mwanao ambayo imeainishwa katika fomu hii ya maelekezo kuepuka usumbufu usio wa lazima.

Nakutakia maandalizi mema na safari njema (Kwa mwanafunzi)

Wako katika ujenzi wa Taifa




**MWL. CHRISTIAN ANTHONY MAKUNGA**
**(MKUU WA SHULE)**

**MAHITAJI MUHIMU YA KUJA NAYO SHULENI**

1. **SARE ZA DARASANI**

◊ Sketi mbili (Damu ya mzee iliyokolea/maroon na kijani mgomba) Linda box ndefu aje nazo,
◊ Mashati meupe mawili mikono mirefu (Aje nayo),
◊ Tai mbili (Neck Tie) rangi za sketi,
◊ Soksi jozi mbili nyeupe (Aje nazo),
◊ Viatu vya ngozi vyeusi visivyo na visigino virefu (Aje navyo),
◊ T-shirt ya kola (Form Six-bluu) moja sare ya shule yenye nembo,
◊ Hijab nyeupe isiyo na mapambo/maandishi (Kwa wanafunzi waislam). Aje nayo,
◊ Sweta moja rangi ya kijani (Kijani mgomba) shingoni "V" aje nalo,
◊ Begi la daftari (Aje nalo).

2. **SARE ZA NJE YA DARASA**

◊ Shamba dress (Gauni) moja rangi ya bluu nyeusi (Dark Blue),
◊ Track suit moja (Kijivu yenye michirizi myeupe miguuni na mikononi) Aje nayo.
◊ Bukta na T-shirt ya mazoezi rangi ya bluu (Aje nazo),
◊ Raba za michezo jozi moja (Aje nazo),
◊ T-shirt moja nyeupe (Shingo ya duara) aje nayo,
◊ Sketi moja nyeusi (Urefu chini ya magoti) aje nayo.
Uwe na mwavuli,

**TANBIHI**

***Mwanafunzi anapaswa kuvaa "track suit" iliyotajwa hapo juu siku anakuja kuripoti shuleni.***

3. **VIFAA VINGINE**

◊ Folder file moja, picha mbili passport size akiwa amevaa shati nyeupe (Background blue). Aje nazo.
◊ Dissect kit moja (Kwa somo la Baiolojia kwa vitendo), Aje nayo.
◊ Laboratory coat moja (Practicals) aje nalo,
◊ Vivuli na nakala za vyeti vya kitaaluma (Result slip na leaving certificate) na,
◊ Kivuli cha nakala ya cheti cha kuzaliwa.

**TANBIHI**

Ni marufuku mwanafunzi kuja na nguo/mavazi tofauti na yaliyoagizwa (Nguo za nyumbani). Mzazi/mlezi unaombwa kuzingatia sana agizo hili.

4. **VIFAA KWA MATUMIZI YA BWENI, JIKONI NA VIFAA BINAFSI**

◊ Mashuka mawili (Light bluu na pink) Aje nayo,
◊ Blanket moja zito rangi yoyote (Aje nalo),
◊ Godoro moja futi 2 ½ aje nalo (Anaweza kununua mji wa Tunduma) na chandarua kimoja kuzuia mbu (Aje nacho),
◊ Ndoo mbili (Moja kubwa na moja ndogo) Aje nazo. Pia; aje na kidumu cha lita 5 kwa ajili ya maji ya kunywa,
◊ Jembe lenye mpini na kwanja (Slasher) aje navyo,
◊ Sahani, kijiko, bakuli na kikombe kwa ajili ya chakula (Aje navyo),
◊Vifaa vya usafi (Hard broom/soft broom, mopa na squizer) (Aje navyo),
◊Sanduku la chuma (Trunker) lenye kufuli imara (Aje nalo),
◊ Mzazi unashauriwa kumpatia mwanao mahitaji binafsi ya kike (Mfano: Taulo za kike bunda zisizopungua tano kwa muhula) na fedha kwa mahitaji yake binafsi (Mwanafunzi hapaswi kumiliki kiasi kikubwa cha fedha bwenini. Utaratibu maalum wa kuwatunzia fedha umeandaliwa).

**TANBIHI**

◊ Kitambulisho cha Bima ya Afya. Mzazi/mlezi unashauriwa kuhakikisha mwanao anamiliki kitambulisho hicho kwani shule haitahusika na gharama za matibabu za kijana wako kwa kipindi chote atakachokuwepo shuleni,

***NI MARUFUKU MWANAFUNZI KUMILIKI SIMU YA KIGANJANI. ATAKAYEKAMATWA KUMILIKI SIMU ATAFUKUZWA SHULE MARA MOJA.***

## 5. ADA NA MICHANGO MINGINE

a. Ada ya shule. Tsh. 70,000/= (Sabini Elfu Tu) kwa mwaka ama Tsh. 35,000/= (Thelathini na Tano Elfu Tu) kwa muhula.
b. Mchango wa taaluma Tsh. 20,000/= (Ishirini Elfu Tu) kwa mwaka(Tsh. 10,000/= kwa muhula),
c. Mchango wa ulinzi, wapishi na vibarua wengine Tsh. 30,000/= (Thelathini Elfu Tu) kwa mwaka,
d. Tahadhari Tsh. 10,000/= (Kumi Elfu Tu) kwa mwaka. Haitarudishwa.
e. Mchango wa ukarabati. Tsh. 30,000/= (Thelathini Elfu Tu) kwa mwaka,
f. Karatasi bunda moja kwa muhula (Ream paper) (Aje nayo),
g. Kitambulisho. Tsh. 5,000/= (Tano Elfu Tu) na,
h. Scientific calculator moja (Aje nayo).
i. Nembo ya shule Tsh.3,000/= (Tatu Elfu Tu),
j. Mitihani ya UTIMILIFU (MOCK) Tsh. 20,000/= (Ishirini Elfu Tu).

**JUMLA YA FEDHA (ADA NA MICHANGO MINGINE) NI TSH 188,000/=** (Mia Moja Themanini na Nane Elfu Tu)

► Jumla ya kiasi tajwa hapo juu ambacho ni kwa ajili ya **ada, taaluma, ulinzi, ukarabati, vitambulisho na tahadhari ziwekwe katika akaunti ya shule namba. 61201100029 NMB. Jina la account ni "CHIKANAMLILO SEC SCHOOL RECURRENT ACCOUNT Njoo na risiti ya Bank (BPS) siku ya kuripoti shuleni yenye jina la mwanafunzi na michango aliolipia.**

Aidha; mzazi/mlezi unashauriwa kumnunulia mwanao vifaa vingine vifuatavyo vya kusomea.

A. Daftari kubwa 10 (Counter book 4 quire). Unashuriwa kumnunulia mwanao daftari nyingi zaidi ya zilizoagizwa kwa matumizi yake binafsi,
B. Kalamu ya wino (Nyeusi/bluu),
C. Kamusi ya Kingereza (Oxford Advanced Learners' Dictionary),
D. Mathematical set (Mkebe),
E. Vitabu mbalimbali vya masomo kulingana na mahitaji ya tahasusi yake. Vitabu vyote vitakuwa mali ya mwanafunzi,

## 6. MAAGIZO MENGINE

A. Ni marufuku mwanafunzi kuvaa ama kukutwa na nguo tofauti na zilizoagizwa katika fomu hii ya maelekezo ya kujiunga na masomo **CHIKANAMLILO SEKONDARI**,
B. Ni marufuku mwanafunzi kutoka nje ya mipaka ya shule bila kibali cha maandishi ya mwalimu mwenye mamlaka (Mfano: mwalimu wa Malezi, bweni, mkuu wa shule, nk),
C. Ni lazima mwanafunzi kutambua wajibu wake kwa kipindi chote atakachokuwepo shuleni. Hivyo; atapaswa kuwa na **NIDHAMU** ya hali ya juu, bidii na jitihada kuhakikisha anafikia malengo yake,
D. Mwanafunzi anatakiwa kuja na fomu ya uchunguzi wa afya yake (Medical examination check up form) ambayo imesainiwa na daktari katika zahanati, kituo cha afya ama hospitali ya serikali na kugongwa muhuri.

## 7. MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa **sheria ya Elimu namba 25 ya mwaka 1978**. Aidha; inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye mamlaka ya elimu nchini. Anapaswa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo ufafanuzi wake zaidi atapata akifika shuleni. Haya ni baadhi tu ya makosa ambayo yanaweza kumfukuzisha mwanafunzi shule.

1. Wizi,
2. Kutohudhuria masomo kwa siku tisini bila taarifa/utoro,
3. Kugoma na kuhamasisha migomo,
4. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu ama wanajamii kwa ujumla,
5. Kumpiga/kupigana na mwanafunzi mwenzake ama kumpiga mwalimu au mtu mwingine,
6. Ulevi ama unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya,
7. Uvutaji wa sigara,
8. Uasherati, uhusiano wa jinsi moja ama kuolewa,
9. Kupata ujauzito ama kutoa mimba,
10. Kushiriki matendo ya uhalifu kinyume na sheria za nchi,
11. Kutembea katika majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni,
12. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya kiganjani katika mazingira ya shule,
13. Kudharau bendera ya Taifa na nembo/alama za Taifa kwa ujumla wake,
14. Kufanya jaribio la kujiua au kutishia kujiua kama vile kunywa sumu, nk
15. Uharibifu wa mali ya/za umma kwa makusudi.

## 8. VIAMBATISHO NA FOMU MUHIMU

a. Fomu ya uchunguzi wa afya (Medical Examination Check up form),
b. Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi
c. Fomu ya mzazi/mlezi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na sheria mbalimbali na kukubali kulipa ada na michango anuai ya shule,

d. Picha nne za wazazi/walezi au watu wa karibu wa mwanafunzi ambao watawajibika kufatilia kwa karibu maendeleo ya mwanafunzi na namba zao za simu za viganjani kwa kipindi chote atakachokuwepo shuleni.

**MAHITAJI YA VITABU VYA KIDATO CHA TANO (V) NA SITA (VI) 2022/2023**

Tunashauri baadhi ya vitabu vifuatavyo mzazi/mlezi umnunulie mwanao ili kurahisisha zoezi zima la ujifunzaji na ufundishaji. Vitabu vitakavyonunuliwa vitakuwa mali ya mwanafunzi. Hivi ni baadhi tu kati ya vitabu vingi vinavyotakiwa kwa tahasusi (Combination) ya "**CBG**".

**1. GEOGRAPHY**

a. General Geography By R.B.Bunnet,
b. Practice Geography for Africa b By Pritchard John M,
c. Regional focal studies for Advance By Msabila, D.T,
d. Map Reading By Mc Master,
e. Physical Geography By Msabila. D.T,
f. Geography An Integrated Approach By David Waugh,
g. An Introduction to Modern economics 4th Edition by Phil Hardwick Khan and John Longmead,
h. Economic Simplified 2nd Edition By N. A. Saleemu,
i. Introduction to Economics By Gupta,
j. A Textbook of Economics By Ashag Hussein,
k. Economic for Advanced Level Paper One and Two and Professional Studies By Ambilikile.

**2. BIOLOGY**

a. Guide to Direction By H.G.Q. Rowert,
b. New Understanding Biology for Advance Level (4th Edition)By Glenn and Suzan Toole,
c. Biology Science 3rd Edition By D.J. Taylor,
d. Plant and Animal Biology Vol I&II; 4th Edition By AE Vines and N. Rees,
e. Functional Approach 4th Edition By M. B. V. Robert,
f. Understanding Biology,
g. Silver Madder,
h. Cell structure and Organization,
i. Principles of Biology,
j. Dissecting set.

**3. CHEMISTRY**

a. Atkins W.P Physical Chemistry; 4th Edition,
b. Atkins W, P 1994; Physical Chemistry,
c. Atkins W.P 2000; General Chemistry Scientific American Books,
d. Barrow G.M; Physical Chemistry; 6th Edition.

**FOMU YA KUKUBALI MASHARTI YA SHULE (FOMU HII IRUDISHWE SHULENI SIKU YA KURIPOTI)**

**A. SEHEMU YA MWANAFUNZI**

1. Mimi (Jina kamili)......................................................wa kidato cha..........2022/2023; ninakubali kujiunga na shule ya sekondari **CHIKANAMLILO** nikiwa mwanafunzi halali wa bweni.
2. Ninaahidi kupata ufaulu wa "Daraja la I ama la II katika mitihani yangu yote (Ya ndani na ya nje-Kitaifa),
3. Nimeyasoma na kuyaelewa masharti yote yaliyoainishwa katika fomu hii ya maelekezo ya kujiunga na elimu ya kidato cha Tano katika shule hii na taratibu, sheria na miongozo ya nchi kwa ujumla.
4. Nipo tayari; uongozi wa shule kunichukulia hatua za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kunirudisha kwa mzazi/mlezi ama kunifukuza shule endapo nitakiuka masharti ya shule na kuvunja sheria za nchi.
5. Bila kulazimishwa! Nikiwa na akili timamu! Nimesoma na kuyaelewa maagizo yote na makatazo! Ninaahidi kuyazingatia.

Sini ya mwanafunzi ...........................................Dole gumba Tarehe ..........................

**B. SEHEMU YA MZAZI/MLEZI**

Mimi (Jina kamili la mzazi/mlezi).......................................................................ninakubali mtoto wangu kujiunga na shule ya **SEKONDARI CHIKANAMLILO** kwa muhula wa masomo wa 2022/2023 kuanzia tarehe ………………………akiwa mwanafunzi wa bweni. Ninakiri kuyasoma maagizo, sheria zote na maelekezo katika fomu hii; na nimeyaelewa vema. Aidha; nipo tayari kulipa michango na ada kama zilivyoainishwa katika fomu hii. Na ninaahidi kushirikiana kwa karibu na uongozi wa shule katika kuhakikisha malengo yanafikiwa. Nitakuwa tayari kumpokea mwanangu endapo ataonekana kukiuka masharti na miongozo iliyowekwa ama kuwa na afya isiyo ridhisha ambayo itahitaji ukaribu na matunzo ya mzazi/mlezi mwenyewe.

**k. Anuani yangu ya kudumu ni:**

| JINA KAMILI | MAHUSIANO(BABA, MAMA,NK) | SIMU YA KIGANJANI | ANUANI YA KUDUMU &SAHIHI |
|---|---|---|---|
| | | | |
| | | | |

ii. Jina na anuani ya kudumu ya mzazi/mlezi wa karibu (Jirani na shule) ambaye shule inaweza kuwasiliana naye katika matatizo anuai ya mtoto/mwanafunzi ni:

| JINA KAMILI | MAHUSIANO(BABA, MAMA, MJOMBA, SHANGAZI, NK) | SIMU YA KIGANJANI | ANUANI YA KUDUMU &SAHIHI |
|---|---|---|---|
| | | | |
| | | | |

**FOMU YA TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI**

a. Jina kamili…………………………………………………………………………………………...

b. Mahali ulipozaliwa…………………………………………………………………………………

c. Tarehe ya kuzaliwa…………………………………………………………………………………

d. Uraia…………………………………………………………………………………………………

e. Anuani ya nyumbani……………………………………………………………………………..

f. Anuani ya mzazi/mlezi (Kama tofauti na hiyo hapo juu) ……………………………………………

g. Jina la mzazi/mlezi………………………………………………………………………………..

h. Kazi ya mzazi/mlezi………………………………………………………………………………

Katika jedwali lifuatalo; jaza taarifa za watu wa karibu (Mzazi/mlezi na ndugu wa karibu) watakaofuatilia maendeleo yako ya kitaaluma na mengine kwa ujumla

| NA | JINA KAMILI | MAHUSIANO/UHUSIANO | SIMU YA KIGANJANI | PICHA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | | | | |
| | | | | |
| 2 | | | | |
| | | | | |
| 3 | | | | |
| | | | | |
| 4 | | | | |
| | | | | |

**TANBIHI:** Watakaondikwa hapo juu ndio watakaohusika kwa karibu kuangalia na kufuatilia maendeleo ya kitaaluma ya mwanafunzi na mambo anuai yakiwepo masuala ya kinidhamu.

i. Dini…………………………………………………………………………

j. Kidato ulichopokelewa…………………………………………………

k. Shule uliyotoka (Kidato cha Nne) ………………………………………..

l. Namba yako ya mtihani (Ya kidato cha Nne)……………………………..

m. Shughuli unazopendelea mbali na masomo ni (Zitaje)……………………………………………………..

n. Wilaya unayotoka…………..…Mtaa/Kijiji……………………Kata ……………………Mkoa……………

o. Matokeo yangu ya kidato cha Nne ni kama yafuatavyo:

| NA | SOMO | DARAJA | NA | SOMO | DARAJA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | | | 7 | | |
| 2 | | | 8 | | |
| 3 | | | 9 | | |
| 4 | | | 10 | | |
| 5 | | | 11 | | |
| 6 | | | 12 | | |

Katika mtihani wa kidato cha nne nimepata daraja (Division)……………..ya point………….

Sahihi ya mwananfunzi……………………………………. Tarehe …………………..

**SCHOOL MOTTO:** ***KAZI, ELIMU, NIDHAMU (KAENI)***

# MOMBA DISTRICT COUNCIL
# CHIKANAMLILO SECONDARY SCHOOL

P.O.BOX 210,
**TUNDUMA-MOMBA.**

DATE…………………

**REF.NO: CHIKANAMLILO.S.S/MEF/VOL1/FV2022**
TO THE MEDICAL OFFICER
…………………………………………………………
…………………………………………………………
…………………………………………………………
Dear sir/Madam;

REF: **REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION FOR** (STUDENT'S NAME IN FULL)……………………………………………………….
(**TO BE FILLED IN THE GOVERNMENT HOSPITAL ONLY**)

Please examine the named above student as to HER fitness for pursuing further education studies at **CHIKANAMLILO SECONDARY SCHOOL** in 2022/2023.

1. Hemoglobin……………………………………………………………………………………….
2. Stool examination…..…………………………………………………………………………….
3. Bilharziasis………………………………………………………………………………………..
4. Urinalysis………………………………………………………………………………………….
5. Tuberculosis (TB) ………………………………………………………………………………
6. Eye ………………………………………………………………………………………………..
7. Abdomen…………………………………………………………………………………………..
8. Asthma……………………………………………………………………………………………
9. Headache ………………………………………………………………………………………….
10. Inability to eat some types of food ……………………………………………………………..
11. Skin diseases……………………………………………………………………………………….
12. Any abnormalities noted above…………………………………………………………………
13. Any clinical complains…………………………………………………………………………
14. Any treatment given or recommended………………………………………………………………..
15. Any STD detected…………………………………………………………………………………..

**NOTE:** In case of unhealthy detected; it is recommended a student to get treatment before coming to school.

**MEDICAL OFFICER'S DECLARATION:** I have examined the above named student and consider that SHE's fit for further studies at **CHIKANAMLILO SECONDARY SCHOOL.**

**NAME AND SIGNATURE**……………………….........................................................................

**DESIGNATION**…………………………………………….,….**STATION**………………………

**OFFICIAL RUBBER STAMP** **DATE**………………